

# Gmail

## Google Ireland Limited (“Google”)

Gordon House, Barrow Street, Dublin 4, Ireland

<https://support.google.com/>

*Itaanza Kutumika Tarehe 21 Disemba, 2020*

### Muhtasari wa Mkataba

- Muhtasari huu wa mkataba unafafanua vipengee muhimu vya huduma tunayoitoa kulingana na matakwa ya sheria ya Umoja wa Ulaya<sup>1</sup>.
- Dhamira yake ni kukusaidia kulinganisha huduma mbalimbali zinazotolewa.
- Maelezo kamili kuhusu huduma tunayoitoa yanapatikana katika hati tofauti.

### Huduma

Gmail ni huduma ya barua pepe inayotolewa katika vifaa na mifumo mbalimbali kupitia kiolesura cha wavuti au programu. Muunganisho wa intaneti unahitajika ili kutuma au kupokea barua pepe kupitia Gmail. Gmail inatolewa na Google kwa kutumia ustadi na umakini unaofaa, ingawa viwango vya chini zaidi vya ubora wa huduma zinazotolewa havijabainishwa.

### Bei

Gmail inatolewa bila malipo na matumizi yake yanapaswa kutii Sheria na Masharti ya Google (yanayopatikana katika <https://policies.google.com/terms>).

### Muda, usasishaji na utamatishaji

Unaweza kupata na kutumia Gmail mara tu baada ya kujisajili. Hulazimiki kutumia Gmail kwa muda fulani uliobainishwa na uko huru kuacha kuitumia wakati wowote.

### Vipengele kwa ajili ya watumiaji walio na ulemavu

Unaweza kufanya kazi na Gmail ukitumia kisoma skrini na mikato ya kibodi na kuweka mandhari ya utofautishaji wa juu. Maelezo zaidi yanapatikana katika <https://www.google.com/accessibility/>.

### Maelezo mengine muhimu

**Usaidizi kwa Wateja:** Usaidizi kuhusu Gmail unapatikana <https://support.google.com/>.

**Migogoro:** Unaweza kupeleka malalamiko kwa mtoa huduma mbadala wa kutatua migogoro aliyeorodheshwa katika <https://ec.europa.eu/consumers/odr/main/?event=main.adr.show2> au mtoa huduma mwingine, kama inavyohitajika na sheria za nchi yako. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye Sheria na Masharti ya Google.

**Matukio ya Usalama:** Google ina mpango wa kina wa kudhibiti matukio wakati wowote, usiku na mchana, ili kutambua na kushughulikia matukio ya usalama au ya faragha bila kuchelewa. Google pia inatoa Orodha ya Masuala ya Usalama ya kukagua ili kukusaidia kudhibiti usalama wako mtandaoni.

**Data Binafsi:** Ili ujisajili kwenye Gmail, unahitaji kutoa jina lako na jina la mtumiaji unalotumia kwenye akaunti yako. Sera ya Faragha ya Google (inayopatikana katika <https://policies.google.com/privacy>) inatoa maelezo zaidi kuhusu data binafsi ambayo Google hukusanya unapotumia Gmail. Sera ya Faragha ya Google si sehemu ya mkataba kati yako na Google wala si sehemu ya muhtasari huu.

---

<sup>1</sup> Ibara ya 102(3) ya Agizo (EU) 2018/1972 la Bunge la Ulaya na la Baraza la Tarehe 11 Disemba 2018 lililounda Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Ulaya (OJ L 321, 17.12.2018, uk. 36).